# SHULE YA SEKONDARI ILUNGA

S.L.P 2318,

MBEYA.

10.12.2020

KUMB. NA ILSS/S.2086/ADM/14/VOL.V/01.

MZAZI WA ………………………………………………………………………………………………….

**YAH : KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA.**

Ninayofuraha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule a sekondari Ilunga mwaka 2021. Anatakiwa kufika shuleni siku ya tarehe 11.01.2021, mwanao akichelewa kuripoti nafasi itachukuliwa na wengine.

**MWANAFUNZI**

Jumuiya ya ILUNGA inakukaribisha.

Unapaswa kutumia muda huu pamoja na mazingira ya shule hii ipasavyo ili hatimaye upate Elimu iliyokusudiwa.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE ZASHULE**

| WAVULANA | | WASICHANA | |
|---|---|---|---|
| I. | Suruali 2 zenye marinda rangi ya blue-kijani na damu ya mzee | I. | Sketi 2 blue-kijani na damu ya mzee mshono marinda urefu kutoka magotini kwenda unyayoni isipungue nchi 12 (cm 30). |
| II. | Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba | II. | Mashati 2 makubwa meupe mikono mifupi |
| III. | Mashati mawili makubwa meupe mikono mifupi | III. | Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba siyo bajaji. |
| IV. | Soksi nyeusi jozi mbili | IV. | Soski nyeupe jozi 2. |
| V. | Sweta 2 blue na damu ya mzee | V. | Hijabu nyeupe (kwa waislam wakike). |
| | | VI. | Sweta 2 blue na damu ya mzee. |

**B.MAAGIZO MENGINE**

1. Madaftari 20 na kalamu za kutosha
2. Begi la kubebea madaftari
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
4. Flat file kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake
5. Mwavuli wakati wa mvua ni muhimu
6. Chakula cha mchana mwanafunzi utahudumiwa na mzazi wako
7. Nauli ya kwenda na kurudi nyumbani, matibabu ni vema umtengee mtoto wako.

**C.VIFAA VYA USAFI**

1. Ufagio 1 (chelewa)

**MUHIMU**

Pamoja na maagizo haya nimeambatanisha

1. Sheria za shule.
2. Fomu ya kupima afya.
3. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri/ kukubaliana na sheria na kanuni za shule.
4. Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi.
5. Fomu ya kukiri kwa mwanafunzi kukubali kujiunga na shule ya ILUNGA SEKONDARI na kanuni na sheria za shule.
6. Fomu ya daktari (mpeleke mwanao hospitali kucheki afya kabla ya kumleta shuleni).

***Ninashauri uyasome maelezo na uyaelewe***

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa na sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Wanafunzi wanahitajika kuishi kwa amani na upendo hapa shuleni. Ugomvi wa aina yoyote ile ni marufuku, kauli zako muda wote zionyeshe busara na upendo. Kuandika matusi kwenye kuta, mbao za madarasani au popote ni uharibifu na ni marufuku.
2. Mali ya shule pamoja na yako binafsi ni lazima itunzwe vyema. Kufanya kitendo chochote ambacho kinaweza kuharibu maliya shule au yako ni kosa kubwa. Kutokana na uzito wa kosa unaweza kufukuzwa shule.
3. Nidhanu inahitajika darasani na nje ya madarasa. Hurusiwi kupiga kelele darasani au kutoka darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa. Mtindo wa kuzomeana ni marufuku hapa shuleni kwani siyo uungwana. Mwanafunzi anapoulizwa lazima anyoshe mkono wa kulia simama unapoulizwa swali au kujibu swali.
4. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kusimama kwa adabu anapoingia mwalimu au mgeni yeyote darasani au shuleni kwa ujumla.
5. Ni lazima mwanafunzi aheshimu ofisi ya mkuu wa shule,walimu na makarani, hakuna ruhusa ya kuingia ofisini na nyumba za walimu na wafanyakazi bila idhini ya mkuu wa shule.
6. Ni lazima mwanafunzi aheshimu bebdera ya taifa na picha za viongozi wa taifa letu, kinyume na hapo mwanafunzi atachukuliwa hatua kali.
7. Mwanafunzi anapozungumza na mwalimu au mkubwa yeyote asiweke mkono mfukoni au kushika kiuno na kubishana, pia mwanafunzi anapoitwa na mwalimu au mkubwa yeyote ni lazima akimbie kwa haraka.
8. Mwanafunzi akishaingia katika eneo la shule haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule hadi anaporudi nyumbani au kwa kibali maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu.
9. Unatakiwa kuhudhuria shughuli zote za shule za ndani na nje ya darasa.
10. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni.
11. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi (nadhifu) muda wote.

## KUFUKUZWA SHULE

Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa shule ni :

i. Wizi.
ii. Uasherati,ubakaji na ushoga.
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
iv. Makosa ya jinai.
v. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vi. Kudharau na kuharibu mali ya taifa .
vii. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
viii. Kuoa au kuolewa.
ix. Utoro.
x. Kufikishwa mahakamani kwa makosa yoyote.
xi. Mwanafunzi asipofika shuleni siku 30.
xii. Kukashifu viongozi wa ngazi zote.
xiii. Uvutaji wa bangi.
xiv. Kutoa mimba.
xv. Kugoma,kuchochea, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu .
xvi. Kukataa adhabu kwa makusudi.
xvii. Kutofuata sheria za shule.

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI ILUNGA**

**FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI**

(*Jaza fomu hii kwa uangalifu*)

1 Jina kamili la mwanafunzi………………………………………………………………………..
2 Tarehe ya kuzaliwa………………………………………Wilaya…………………………………..
3 Kabila ……………………………….Uraia……………………Dini………………………………..
4 Jina la mzazi…………………………………………………………………………………………..
Anuani ya mzazi……………………………………………………………………………………..
Kazi ya mzazi…………………………………………… namba ya simu……………………

*(sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao)*

5 (a) Jina la mlezi………………………………………………………………………………………
(b) Uhusiano kati ya mlezi na mwanafunzi………………………………………………………
(c) kazi ya mlezi……………………………………………………………………………………..
(d) anuani ya mlezi ……………………………….namba ya simu……………………………

6. Shule atokayo mwanafunzi……………………………………………………………………

7. Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi?…………………………………………..

8. Maelekezo ya mwanafunzi……………………………………………………………………..

9. Ujuzi(stadi)mwingine…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA SEKONDARI ILUNGA**

**FOMU YA KUKUBALI**

1. Mimi ……………………………….............msichana/mvulana nimekubali kuingia kidato cha kwanza…………………….katika shule ya sekondari ilunga kama mwanafunzi wa kutwa tarehe ……………………………………………………..nitafika shule bila kuchelewa.
2. Nitatii sheria za shule na nitaishi maisha mazuri .Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.
3. Saini ya mwanafunzi…………………………………..tarehe……………………………

**SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI.**

1. Mimi …………………………………………………………nimekubali mtoto wangu…………………………………………………..........asome katika shule ya sekondari ilunga kuanzia tarehe …………………………………………………………….
2. Ninaahidi kumpatia vitu vyote anavyoatakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na uwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.
4. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya sekondari ilungakama mwanafunzi wa kutw,na ataendelea hivyo hadi kumaliza kidato cha nne.naelewa kuwa nafasi katika shule za bweni ni haba sana.hivyo mm wala mwanangu hatutamsumbua mkuu wa shule kwa vyovyote kuhusu mipango ya malazi au uhamisho kwenda shule ya bweni.
5. Ninaahidi kuwa mwanagu atafanya shughulizote za shule za kujitegemea (EK) kwa mikono kwa juhudi na maarifa.

Jina la mzazi…………………………………………………………………………………….
Sahihi…………………… tarehe……………………

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING

ILUNGA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 2318,
MBEYA.

Date …............
THE MEDICAL OFFICER
………………………………..
………………………………..
………………………………..

**PART "A"**

Mr, miss…………………………………………………………………………………………….
Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time student in the school. The examination should include the following categories

1. Hemoglobin ……………………………………………………………………………..
2. P. V Bleeding …………………………………………………………………………
3. Sight ……………………………………………………………………………………….
4. Blood pressure ……………………………………………………………………….
5. Urine for sugar and pregnancy tests…………………………………………….
6. Stool for routine examination ………………………………………………………..
7. Asthma ……………………………………………………………………………………
8. Skin diseases …………………………………………………………………………
9. Leprosy …………………………………………………………………………………
10. Any deformity ………………………………………………………………………….
11. Epilepsy …………………………………………………………………………………..
12. Pulmonary tuberculosis …………………………………………………………
13. Neurosis …………………………………………………………………………………

14. Venereal diseases …………………………………………………………………….
15. Other serious diseases ……………………………………………………………..

**PART "B"**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government medicalofficer)

1. I have examined the ………………………………………………………………..
   above named pupil and consider that he/she is physical fit/unfit and metally fit/unfit for full schooling.
2. Other comments
   ……………………………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………………………
   ………………………

Date ……………………………                                        ………………………………….

Signature